

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**

**MKOA WA NJOMBE**

**Simu: 026-2968833**

**Faksi: 026- 298832**

**E- mail: td@njombetc.go.tz**

**Tovuti: www.njombetc.go.tz**



**S.L.P 577,**  
**NJOMBE.**

**Njombe, 19/04/2019**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

UFAPANUZI WA HABARI ILIYOANDIKWA KWENYE MITANDAO YA KIJAMII (BLOGS) YA DAR MPYA YA TAREHE 18/04/2019 YENYE KICHWA CHA HABARI **“AGIZO LA RAIS MAGUFULI KUKAMILISHWA KITUO CHA MABASI NJOMBE MJINI NDANI YA SIKU 30 HALIWEZI KUFANIKIWA”** NA ILIYOCHAPISHWA KWENYE MTANDAO (BLOG) YA MPEKUZU TAREHE 19/04/2019 YENYE KICHWA CHA HABARI **“MWANZINGA: AGIZO LA RAIS MAGUFULI KUKAMILISHWA KITUO CHA MABASI NJOMBE MJINI NDANI YA SIKU 30 HALIWEZI KUFANIKIWA.”**

Halmashauri ya Mji Njombe inapenda kutoa ufafanuzi kuhusu taarifa iliyoandikwa katika mitandao ya Kijamii (Blogs) yenye jina la **Dar Mpya** ya tarehe 18/04/2019 na iliyoandikwa tarehe 19/04/2019 kwenye Blog ya **Mpekuzi** yenye vichwa vya habari kama vinavyosomeka hapo juu kuwa ni ya upotoshaji, imelenga kuleta sintofahamu kwa jamii, na ipuuzwe.

Katika mahojiano yaliyofanyika siku ya tarehe 18/04/2019 na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Njombe Ndg. Edwin Mwanzinga kuhusu kukamilika kwa ujenzi wa stendi mpya ya Njombe ni kwamba, Mwenyekiti alifafanua kuwa stendi hiyo itakamilika kwa mujibu wa tarehe ya mkataba ambayo ni 30/04/2019 na shughuli zitakazosalia za ukamilishaji zitafanyika ndani ya siku zilizoongezwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kama alivyoagiza kwenye ziara yake ya kikazi tarehe 10 Aprili akiwa Mkoani Njombe ambapo ni kufikia tarehe 10, Mei 2019. Mahojiano hayo hayakuelezea kutokutekelezeka kwa agizo hilo kama ilivyoripotiwa.

Msimamo wa Mwenyekiti na Halmashauri ni kwamba ujenzi wa kituo hicho utakamilika ndani ya wakati kulingana na mkataba na kwa mujibu wa siku ambazo Mhe. Rais ameziongeza.

Halmashauri ya Mji Njombe inasikitishwa na taarifa hiyo na inautaarifu umma kuzingatia maelezo haya.

**Imetolewa Na,**

**Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Uhusiano,**  
**Halmashauri ya Mji Njombe.**